

**UTETEZI WA WAZI WA
DR. HARRISON MWAKYEMBE
Juu ya hoja ya mgongano wa kimaslahi**



MACHI 20, 2009

Na. M. M. Mwanakipiji

Utangulizi:

Ndani ya siku hizi chache tumeshuhudia hoja ambazo zina hisia nyingi na ambazo naamini kwa kiasi kikubwa ni sehemu ya yale yale mapambano ya kifikra. Hoja hizi zimejengwa hasa dhidi ya Dr. Harrison Mwakyembe Mbunge wa Kyela na aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Bunge iliyochunguza mkataba wa Richmond ambayo ripoti yake Bungeni ilisababisha aliyekuwa Waziri Mkuu kujiuzulu kufuatia kashfa ya kampuni feki ya Richmond.

Kuanzia matukio yale ya kihistoria ya mwaka jana hadi leo hii kumekuwepo na majaribio ya kila aina ya kumdhalilisha na kumbomoa Dr. Mwakyembe na ninaamini hili la sasa hivi limedhaniwa kuwa ndilo linaloweza kufanikiwa. Kuanzia suala la kukatiwa maji na DAWASCO mwezi wa nne mwaka jana. Wakati ule kama ilivyo sasa walioathirika na ripoti ya Mwakyembe Bungeni walionesha kufurahia kuwa hatimaye kumbe na Dr. Mwakyembe naye ni fisadi.

Katika jaribio jingine la sasa kuna imani ya kwamba hatimaye safari hii wamempata. Hata hivyo hilo ni kundi moja tu.

Kuna kundi la pili la wale ambao wanaamini katika maadili ya uongozi ambao wanaamini kuwa kwa jinsi walivyosoma na kutambua kuwa Dr. Mwakyembe naye ni mmiliki wa kampuni ya kufua umeme basi alitakiwa kutangaza maslahi hayo katika Kamati Teule (wakati wa kuzungumza Bungeni mwaka jana) na pia katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo yeye ni mjumbe. Hawa wanaamini Dr. Mwakyembe amevunja maadili na amekiuka miiko fulani.

Hawa naweza kusema wanaongozwa na kanuni.

Ni makusudio yangu kumtetea Dr. Mwakyembe dhidi ya makundi yote mawili na kuonesha kuwa hoja zao ni za kuvutia masikio lakini hazina msingi, ni dhaifu na tukiziangalia kwa karibu tutaona zina makosa mengi. Kwamba, makundi yote mawili yamekosea kwa hoja zao na kwa ushahidi wanaotoa. Tafadhali fuatana nami katika utetezi huu wa wazi wa Dr. Harrison Mwakyembe.

Unapofuatana nami hakikisha unaangalia sana matumizi ya maneno yangu kwani najitahidi kuchagua maneno vizuri kutaka kumaanisha kile ninachokisema na kusema ninachomaanisha. Ukikosea stepu usisite kurudi nyuma kunipata vizuri.

Kwa wale wageni na makala zangu za utetezi hii siyo makala ya kwanza au hoja ya kwanza ya utetezi. Huko nyuma nilisimama kumtetea marehemu Amina Chifupa baada ya “kunyamazishwa”, nimemtetea Waziri Sofia Simba, na nimewatetea mabinti wa Nyegezi kina Nsia Swai. Na huu utetezi hautakuwa wa mwisho kwa mtu yeyote ambaye dhamira yangu inanituma kuamini kuwa aidha anaonewa au kutokana na nguvu zaidi anawekwa mahali ambapo hawezi kushinda.

Kiini cha Utetezi.

Utetezi wangu kwa kiasi kikubwa unafanana na utetezi wa Dr. Mwakyembe mwenyewe mbele ya waandishi wa habari juzi lakini nitaenda mbali zaidi na kuonesha kwa kupitia mantiki kuwa baadhi ya hoja zinasimama au kushindwa kutegemea na maneno machache ya Kanuni za Mijadala Bungeni.

Kanuni za Bunge inayozungumzia taratibu za mijadala, Ibara ya 61() inasema hivi kwa “*wakati wa majadiliano bungeni au kwenye kamati yoyote ya Bunge, mbunge hataruhusiwa kuzungumzia jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi binafsi nalo ya kifedha*”. isipokuwa maslahi

*hayo, na kwa sababu hiyo, itakuwa ni lazima kwa mbunge ye yote anayetaka kuzungumzia jambo hilo bungeni au kwenye kamati yoyote ya Bunge, kusema kwanza jinsi anavyohusika na jambo hilo na kutaja kiwango cha maslahi ya **kifedha (pecuniary interests)** aliyonayo kuhusiana na jambo hilo kabla ya kuanza kuzungumzia jambo hilo”* Msisitizo wangu.

Msomaji nakuomba uangalie sana maneno hayo hapo juu kwani tutayarudia sana huko mbeleni hasa maslahi ambayo Mbunge anatakiwa kuyafunua kabla hajazungumzia jambo.

Maana pana ya mgongano wa maslahi

Tatizo kubwa ambalo nimeliona ni kuwa uelewa wetu wa dhana nzima ya mgongano wa maslahi ni mdogo kwa maana ya kwamba tumechukulia maana pana sana ya mgongano wa maslahi kiasi kwamba tukiikubali hakuna Mtanzania yeyote anaweza kufanya jambo lolote na kama ni Bungeni wabunge wote itabidi wajiuzulu siyo tu kutoka kwenye Kamati bali ubunge wenyewe! Nitawaonesha nitakapojibu hoja za kundi lile la pili.

Kwa upana wake, mgongano wa maslahi hutokea pale ambapo mtu binafsi anakuwa katika nafasi fulani ambayo inaweza kumpa manufaa ya aina fulani ambayo asingeweza kuyapata kama asingekuwa katika nafasi hiyo. Manufaa hayo ni kinyume na manufaa ya taasisi, kundi, au chombo fulani ambacho kinawakilisha maslahi mengine. Hivyo katika mgongano wa maslahi ulivyo maslahi ya mtu binafsi yanagongana na maslahi ya taasisi, jumuiya au kundi fulani.

Kwa mfano, Mwalimu wa shule ya msingi ambaye anafundisha somo la hesabu anapoamua kuanzisha ‘tuition’ ya hesabu kwa wanafunzi wale wale anaowafundisha shuleni. Maslahi yake ya kujipatia kipato zaidi yanagongana na maslahi ya shule kuwapatia wanafunzi elimu kwa bei nafuu. Lakini mwalimu huyo huyo akifungua tuition ya hisabati kwa wanafunzi wasio wa shule yake anaweza asiwe na mgongano na shule yake!

Sasa migongano ya maslahi ipo mbele zetu karibu kila siku na ni jukumu letu kuitambua na kuona jinsi ya kuiepusha. Katika sheria zetu za hivi karibuni tumejaribu sana kuhakikisha migongano ya maslahi haitokei au inaepukwa. Kwa mfano, tumekataza madiwani katika halmashauri zetu kuwa wanagombea tenda zinazotolewa na halmashaurii hizo hizo wakati wao wenyewe ndiyo wasimamizi wa tenda!

Hata hivyo, taasisi mbalimbali zinamaana yake ya mgongano wa maslahi na hivyo kuweka katika taratibu zake na wanasema “kama jambo hili likitokea basi ni mgongano wa maslahi na tutashughulikia hivi”. Kwa maneno mengine, maana ya mgongano wa maslahi ni pana mno na ni jukumu la taasisi kuweka mipaka yake. Bunge la Jamhuri ya Muungano limeweka mpaka katika uelewa wake wa mgongano wa maslahi linapokuja suala la kuchangia Bungeni.

Mpaka ni huo uliopo hapo juu kwenye “kiini cha utetezi”. Kuwa, katika mijadala Bungeni maslahi yanayotakiwa kutangazwa na mbunge ni yale ya “kifedha”. Sasa wangeweza kuweka mipaka mingine mingi n.k lakini walichosema ni kuwa Mbunge hatozungumzia jambo ambalo ana maslahi ya kifedha bila “kusema kwanza jinsi anavyohusika na jambo hilo na kutaja kiwango cha maslahi ya **kifedha (pecuniary interests)** aliyonayo kuhusiana na jambo hilo kabla ya kuanza kuzungumzia jambo hilo”.

Hivyo kama kuna maslahi yoyote nje ya yale ya kifedha Mbunge wa Jamhuri ya Muungano halazimishwi kusema lolote. Ni lazima kuwe na maslahi ya kifedha ndipo Mbunge anatakiwa kusema. Bila kuweka mpaka wa uelewa wa mgongano wa maslahi basi mtu atakuwa na mgongano wa maslahi hata akiamua kuamka tu kitandani kwenda kazini!

Majibu kwa hoja za gazeti la Mtanzania.

Katika gazeti la Mtanzania lililoibua suala la umiliki wa Dr. Mwakyembe pamoja na wenzake katika kampuni ya Powerpool kuna hoja tano zinazotolewa kuwa Mwakyembe alikuwa na mgongano wa maslahi wakati anachunguza kampuni ya Richmond wakati anaongoza Kamati Teule ya Bunge.

Ukisoma habari za gazeti hilo Toleo No. 4689 la tarehe 15 Machi 2009 lenye kichwa cha kichwa cha habari "Dk. Mwakyembe Aumbuliwa" kuna hoja tano ambazo zimetolewa kuonesha kuwa Dr. Mwakyembe alikuwa na mgongano wa maslahi wakati akiwa Mwenyekiti wa Kamati Teule na alitakiwa kutangaza mgongano huo palipo alipotoa ripoti yake. Hoja zote tano zinahusiana na kampuni ya Richmond/Dowans.

Hoja ya kwanza:

“Wachunguzi wa mambo wanaamini kuwa ushujaa wa Dk. Mwakyembe kuishambulia kampuni ya Richmond, na baadaye Dowans, unatokana na mgongano wa kimaslahi.”. Tatizo ni kuwa hawasemi ni maslahi gani wanazungumzia ambayo Mwakyembe angeyapata kwa kuichunguza Richmond na kuipinga Dowans.

Hoja ya Pili:

“(wachunguzi hao) wanasema Dk. Mwakyembe na wenzake wanapinga Dowans kununuliwa ili wapate mwanya wa kuuza umeme utakaozalishwa na kampuni yao ya Power Pool East Africa Limited...” Hapa wanasema kwamba, leo hii serikali isiponunua mitambo ya Dowans basi Dr. Mwakyembe na kampuni ya Powerpool East Afrika watauza umeme kitu ambacho kilitakiwa kufanywa na Dowans. Tatizo hapa ni kuwa kampuni ya kina Mwakyembe hata kuweka pangaboi moja la kuzungushwa na upepo halipo. Sasa huo umeme ambao unaweza kuwanufaisha leo unapatikana wapi? Kama Dowans ikinyimwa sasa hivi na kampuni nyingine ikaingia na kuziba pengo hilo kina Mwakyembe wananufaika vipi?

Hoja ya Tatu:

“Dk. Mwakyembe na wenzake walianzisha kampuni yao kabla ya ujio wa kampuni iliyozua utata mkubwa wa Richmond. Matarajio yao yalikuwa kwamba wazalishe umeme na kisha waiuzie Tanesco, lakini ujio wa Richmond ulionekana kutaka kuwakwaza.” Sasa hapa tujiulize, kampuni ya kina Mwakyembe imeanzishwa 2004, Richmond imekuja 2005 na kampuni ya kina Mwakyembe hata fedha za kuanzisha mradi hawana wanatishiwa vipi? Kama wakati kampuni ya kina Mwakyembe ingekuwa imeanza uzalishaji wakati ule na Richmond inakuja basi hapo kunakuwa na mgongano kwani maslahi ya kifedha ya kina Mwakyembe yanatishiwa na ujio wa Richmond.

Sasa kama kampuni yao haiko katika nafasi ya uzalishaji, na mwaka huo sidhani kama hata walikuwa na kiwanja (yaani walikuwa kwenye daftari huko BRELA), na haina mtaji wa kuanza biashara hiyo ni maslahi gani ya kifedha yanatishiwa na ujio wa kampuni ya Richmond ambayo tuliambiwa ingeweza kuanza uzalishaji “miezi michache tu”?

Hoja ya Nne:

“Akiwa Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Bunge iliyochunguza Richmond, hakuwahi kutangaza hata mara moja mgongano wa kimaslahi aliokuwa nao kwenye suala hilo.” Sasa hapa ndiyo kujaribu kutafuta simba kwenye kichuguu cha mchwa! Wanapoandika hili bila ya shaka wanafikiria hiyo ibara ya 61 ya taratibu za Bunge. Tatizo ni kuwa ibara hiyo inasema “maslahi ya kifedha”.

Sasa kama hakuwa na maslahi ya kifedha (kwa mfano, Richmond wakiondoka kampuni yangu itaanza kuuza umeme) ni kitu gani walitaka aseme? Kwamba, “jamani mimi nina kampuni inayotarajia kuanza kufua umeme mwaka 2015”. Sasa ni mgongano gani wa maslahi kati ya kampuni hiyo na kampuni ambayo imepewa mkataba wa miaka miwili wakati huo?

Mgongano hapo ungekuwepo kama Mkataba wa Richmond ungekuwa ni wa muda mrefu, muda ambao ungeingiliana na kuanza kwa uzalishaji wa kampuni ya Powerpool.

Hoja ya Tano:

“Dk. Mwakyembe, akionekana kuwa msitari wa mbele kuhakikisha kuwa mitambo ya kampuni ya Dowans hainunuliwi, anashupalia msimamo huo kutokana na mgongano wa maslahi.” Hapa wanataka kusema kuwa endapo mitambo ya Dowans haitanunuliwa Dr. Mwakyembe atanufaika kwa namna fulani. Sasa nimejiuliza atanufaikaje wakati kampuni yake haiko katika uwezo wa aina yoyote wa kuanza kuzalisha umeme?

Lakini cha kushangaza ni kuwa wanataka watu waamini kuwa sababu pekee ya kupinga mkataba wa Dowans kwa Mwakyembe ni kuwa ili anufaika! Je yawezekana anapinga kwa sababu Dowans nayo ni kama Richmond imeingia nchini kiulaghai? Kwamba imeingia nchini kwa kupigiwa debe na Rostam Aziz Mbunge wa Igunga ambaye ni Mmiliki wa gazeti la Mtanzania? Je yawezekana gazeti la Mtanzania nalo lilitakiwa kutangaza maslahi yake kwa sababu linahusiana na mtu pekee aliyemvutia rafiki yake mmiliki wa Dowans kuja Tanzania na mitambo hiyo na kuwa msimamo wa Mwakyembe unatishia maslahi ya boshi wao!?

Hivi endapo serikali ikiamua kuitaifisha mitambo ya Dowans (yaani kuichukua kwa nguvu bila kuilipia) ni nani atakayeathirika zaidi na maslahi yake ya kifedha kuwa mashakani? Jibu wala halihitaji kwenda mbali ni Rostam Aziz na rafiki yake mkubwa na mshiriki wa biashara Brig. Gen. Suleiman Al-Adawi!

Hivyo pasipo shaka yoyote ile kwenye suala la uchunguzi wa Richmond/Dowans hakukuwa na maslahi yoyote ya kifedha ya Dr. Mwakyembe ambayo yalitishiwa na ujio wa Richmond. Bila maslahi ya kifedha kama ilivyo kwenye kanuni za Bunge hakuna mgongano wa maslahi wa kuutangaza.

Kama Bunge au Wabunge wanataka kila mtu atangaze “maslahi yote” aliyonayo ni jukumu lao kubadili sheria, lakini sheria ilivyo sasa Mwakyembe anaibuka na ushindi. Isipokuwa kama kuna mtu anaweza kutuonesha maslahi ya kifedha ya Mwakyembe ambayo ameyapata baada ya Richmond kutupiliwa na mkataba wa Dowans kufutwa.

Mgongano wa kimaslahi haupo kwa sababu ya umiliki kama wangetaka iwe hivyo Wabunge wangesema wazi kuwa “mbunge atatangaza maslahi ya umiliki, hisa, mahusiano n.k katika jambo analotaka kuzungumzia!”. Hawakusema hivyo, wamesema “maslahi ya kifedha”.

Kimsingi hoja zile zote zilitaka kuacha taswira kuwa Richmond ilionewa na Dr. Mwakyembe! Tatizo ni kuwa maamuzi yaliyotolewa hayakuwa ya Mwakyembe peke yake bali Kamati Teule, na yaliletwa Bungeni, yakajengewa hoja Bungeni, Lowassa na wenzake walikasirika, walamua kususa na kuamua kujiuzulu. Walishindwa kujibu hoja na badala yake tangu wakati ule wameamua kuleta vioja.

Kama wanaamini wameonewa au hawakutendewa haki wapeleke hoja zao Bungeni na kina Mwakyembe na Selelii wameshasema mara kadhaa kuwa kama itaoneshwa kuwa wamewaonea wako tayari kuwajibika kisiasa.

Majibu kwa wale wanaaomini mgongano wa maslahi wa Kamati

Upande huu sasa hivi unaongozwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe Mbunge wa Kigoma Kaskazini na yawezekana pia wabunge wengine (tukiamini habari za gazeti la Daily News). Kimsingi, hoja yao ni kuwa Mwakyembe kama mmoja wa wamiliki wa kampuni hii ya nishati hakustahili kuwemo kwenye kamati ya nishati kwani anamgongano wa maslahi.

Hata hivyo, hakuna mahali popote panaposema kuwa umiliki wa kampuni fulani ni kigezo cha kutokuwa mjumbe wa kamati inayohusiana na sekta ya kampuni hiyo. Ibara tunayozungumzia inasema “maslahi ya kifedha” na maslahi ya kifedha siyo lazima yapatikane kwa umiliki.

Lakini tatizo kubwa zaidi ni kuwa sheria zao wenyewe Bungeni zinaelezea taratibu ya kuteua wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge. Toleo nililolalo ni la zamani (kabla ya mabadiliko ya mwaka jana) nalo linasema hivi kuhusu uteuzi wa wajumbe wa Kamati za Kudumu (kama hiyo ya Nishati na Madini) kuwa Spika atetua wajumbe wa kamati hizo kwa kuangalia vigezo mbalimbali kigezo kimoja ni “have regard to the need for each Committee to have Members with experience or special skills in respect of the duties and responsibilities of the respective Committee.” Yaani “ataangalia mahitaji ya kila Kamati kuwa na wajumbe wenye uzoefu na ujuzi na kazi na majukumu ya hizo kamati”.

Kwa maneno mengine, Spika akimteua Daktari wa watu kuwa mjumbe wa Kamati ya Afya kama alivyompatia Dr. Lucas Siyame hajatengeneza mgongano wa maslahi; Kama Spika akimteua Dr. Kigoda kuwa mjumbe wa kamati ya Uchumi na Fedha wakati ni mfanya biashara na anapata nafasi ya kujua mambo mbalimbali ya uwekezaji n.k haiwezekani kuwa ni mgongano wa maslahi?

Taratibu zao wenyewe (bungeni) zinasema unaangalia uzoefu na ujuzi wa wajumbe, sasa ukiwa na Kamati ya Afya ambayo haina daktari hata mmoja, au kamati inayosimamia Elimu ambayo haina mwalimu hata mmoja; yaani yote yafanyike kwa sababu ukimuweka mwalimu, daktari au mfanyabiashara kwenye kamati zinazohusiana na fani zao au shughuli zao unaleta mgongano wa maslahi si itakuwa vurugu tupu?

Wangapi kati ya wabunge walioko kwenye kamati mbalimbali wana biashara, hisa, n.k zinazohusiana na mambo wanayoyashughulikia kwenye kamati? Ni mara ngapi watu hao wametakiwa kutangaza maslahi yao hata kama hawana kliniki, hawana shule au kikampuni chochote kile? Wangapi kati yao nao wameanzisha kampuni zilizoko kwenye makaratasi BRELA?

Lakini tatizo jingine hapa ni kuwa watu wanataka Mwakyembe ndiyo aonekana amekiuka maadili wakati sheria wameziandika wao Bungeni na kipimo wanachompimia Mwakyembe hakijawahi kupimiwa mtu mwingine. Kwamba, mtu akiwa na uzoefu au ujuzi wa kitu fulani hatakiwi kuingia kwenye Kamati ya Bunge inayohusiana na ujuzi au uzoefu huo.

Lakini tatizo lao kubwa kwa Mwakyembe kuwa mjumbe wa Kamati ya Madini ni kuwa kwa maneno ya Zitto “Kosa kubwa ninaloliaona, kama daktari anamiliki kampuni ya umeme, ni lile la yeye kuwa makamu mwenyekiti wa kamati ya nishati na madini au hata kuwa mjumbe wa kamati ile. Hii ni total conflict of interest maana kamati ile ndio inashughulikia sera za umeme.”

Sasa hili kwa wengine wamelipeleka mbele kuwa Mwakyembe kwa vile ni mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na mmiliki wa kampuni ya kufua umeme (ambayo hata hela ya kuanzisha

mradi kwa maneno haya haina) ni kuwa anapata unfair advantage ya kujua mambo mbalimbali yanayoendelea kwenye sekta ya nishati.

Hivyo watu hao wanaamini kuwa Mwakyembe anaweza kupata taarifa za mikataba na mipango mbalimbali na hivyo kuweza kuitumia kwenye mipango ya kampuni yake.

Tatizo la mtazamo huo ni kuwa Mwakyembe kupata taarifa hizo hazitegemei kuwa mjumbe wa Kamati. Yeye kama Mbunge tayari anapata taarifa za Bunge na taarifa za kamati nyingine zote za Bunge!

Taratibu za Bunge zinasema wazi kuwa shughuli za Kamati za Bunge ziko wazi kwa wananchi hasa baada ya mabadiliko ya 2007. Huko nyuma mambo hayo yalikuwa siri siku hizi kuna uwezekano wa mikutano ya Kamati hizi kuwa wazi kwa mwananchi yeyote na kufanyika mbele ya kamera.

Zaidi ya yote taratibu za Bunge ziko wazi kuwa mtu yeyote (awe Mbunge au vinginevyo) anaweza kuona taarifa zozote za Bunge ambazo zinahifadhiwa kwa mujibu wa sheria na Katibu wa Bunge. Ina maana ya kwamba, siyo tu Mwakyembe ambaye anaweza kunufaika na ripoti za Kamati ya Madini na Nishati bali pia Msabaha, Selelii, Zitto, Malecela, na Mwajuma na Rebecca na Rostam na Serukamba.

Kwa maneno mengine, kwa kuwa kwake mjumbe wa Kamati ya Madini na Nishati Mwakyembe hana faida yoyote au kunufaika na ujuzi wowote wa jambo ambalo Mbunge mwingine naye hana awe mjumbe wa kamati au la! Anachokiona Mwakyembe kwenye Kamati yake kinaweza kuonwa na mtu mwingine yoyote yule siyo siri fulani hivi.

Kimsingi utaona kuwa hoja zote mbili hazina msingi. Ukizichunguza kwa karibu utaona kuwa hazina nguvu vile vile. Ni hoja zinazotokana na kudhania kuliko hali halisi.

Dr. Mwakyembe hajavunja utaratibu wowote wa Bunge, hana maslahi yoyote ambayo kwa kuwa kwake mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini anazipata ukilinganisha na kutokuwa mjumbe.

Kama taarifa zote za kamati mbalimbali zinapatikana kwa mbunge yoyote ile hata asiye mjumbe wa kamati yoyote (ndiyo maana wabunge fulani huwaoni kwenye kamati yoyote haina maana hawana taarifa za kamati hizo) basi ipo haja ya kuwatimua wabunge wote.

Maana wote hawa wako katika nafasi ya kunufaika kwa taarifa za mambo ambayo Mtanzania wa kawaida hana. Wabunge wana nafasi ya kuhoji watu, kuitisha nyaraka n.k na kutembelea mahali popote hata viwanda vya wapinzani wao! Sasa kama hii faida ni conflict of interests, basi Wabunge wote wajiuzulu nafasi zao wakiongozwa na Dr. Harrison Mwakyembe akifuatiwa na Rostam, Lowassa, Malecela, Mkumba, Spika na kama tunataka kwenda mbali zaidi watanguliwe na Rais mwenyewe kwani hakuna mtu mwenye kujua mengi kuhusu mambo mbalimbali ya uwekezaji na miradi mbalimbali mikubwa kama yeye.

Vinginevyo, Wabunge wenyewe waangalie mswada wa Zitto kuhusu maadili, wabadilishe taratibu zao, waangalie sheria ili hatimaye waje na utaratibu ambao ni wa haki, ni wa wazi na usio na mwelekeo wa kumlenga mtu fulani.

Ukipenda kupata nakala ya bure ya kijarida chetu cha Cheche kila wiki na kutoa maoni yako niandikie: mpariri@klhnews.com na tembelea tovutu yetu: <http://www.mwanakijiji.com>

* * * SAY NO TO DOWANS! ***